TANGAZO LA SERIKALI Na. 50J la tarehe 28/1/2025

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA ITOKANAYO NA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA KIFEDHA ZA KIGENI KATIKA MRADI WA UANZISHAJI WA MTAMBO WA UKAMUAJI NA UFUNGASHAJI WA SUKARI KWA KAMPUNI YA KILOMBERO SUGAR YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Riba Itokanayo na Mikopo kutoka Taasisi za Kifedha za Kigeni katika Mradi wa Uanzishaji wa Mtambo wa Ukamuaji na Ufungashaji wa Sukari wa Kampuni ya Kilombero Sugar ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 28 Juni, 2024.

Msamaha

**2**. Kodi ya zuio inayopaswa kulipwa na Kampuni ya Kilombero Sugar katika riba itokanayo na mikopo kutoka tasisi za kifedha za nje kwa ajili ya utekekelezaji wa mradi wa Uanzishaji wa Mtambo wa Ukamuaji na Ufungashaji wa Sukari inasamehewa.

Ukomo

**3**. Amri hii itafika ukomo wake tarehe 31 Mei, 2027 kwa mujibu wa kipengele cha 3.3 cha mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Kilombero Sugar na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 23 Juni, 2023.

Dodoma,
31 Disemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*